Hake Muhtasari 05K, 2014

# Mwaka mmoja wa Matokeo Makubwa Sasa

## Je tunatekeleza Ipasavyo?

**Utangulizi**

Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, kwa kiingereza Big Results Now (BRN), ni sehemu ya jitihada za serikali ya Tanzania kuinua uchumi toka nchi yenye uchumi wa chini mpaka nchi yenye uchumi wa kati. Katika kutekeleza mpango huu serikali imeanza na wizara sita: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikiwa ni mojawapo, Wizara zingine ni Kilimo, Maji, Usafirishaji, Fedha na Nishati. Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa umelenga katika kujizoesha na kufuata njia mpya za ufanyaji kazi katika muda maalumu uliopangwa katika utoaji wa huduma ili kuleta matokeo yanayokusudiwa kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Tathmini hii fupi inajaribu kuainisha mafanikio ya utekelezaji wa BRN katika sekta ya elimu kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu ilipoanza rasmi mwaka 2013 kwa kulinganisha na malengo yaliyowekwa kwa mwaka 2014.




**Malengo ya BRN kwenye sekta ya Elimu mwaka 2013 na 2014**

- Kuongeza ufaulu wa elimu ya msingi na sekondari kufikia asilimia 70 mwaka 2014
- Kutoa ruzuku yote kwa kila mwanafunzi
- Kutoa Mafunzo ya Uongozi kwa walimu 19,035 kufikia Septemba 2013
- Mafunzo kwa walimu 12,300 juu ya kufundisha KKK
- Kujenga nyumba za walimu 500 kwa shule za sekondari
- Kukarabati Miundombinu kwa shule 1,200 za sekondari
- Kila mwanafunzi kuwa na vitabu 6

**Hali ya Ufaulu wa Mitihani wa Darasa la Saba na Kidato cha Nne**

Wizara ya Elimu imebainisha kuongeza kiwango cha ufaulu kwa shule za sekondari na msingi kufikia asilimia 60 mwaka 2013, asilimia 70 mwaka 2014 na asilimia zaidi ya 80 kwa mwaka 2015. Chati namba 1, inaonesha kuwa ufaulu umeongezeka kwa shule za msingi na sekondari. Mwenendo ni mzuri zaidi kwa shule za sekondari ambapo ufaulu umeongezeka toka asilimia 50.6 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 58 mwaka 2013. Hii inamaanisha lengo la ufaulu kwa sekondari kufikia asilimia 60 kwa mwaka 2013 limefanikiwa kwa asilimia karibu 79. Lakini changamoto inabaki kuwa ufaulu wa sekondari si wa kujivunia kwa sababu matokeo ya mtihani wa mwaka 2013 yametumia viwango vipya vya madaraja, na hivyo hatuwezi kuyalinganisha na matokeo ya mwaka 2012. Japo ufaulu umeongezeka pia kwa elimu ya msingi toka asilimia 30.7 mwaka 2012 hadi asilimia 50.6 Hatahivyo ufaulu wa elimu ya msingi si wa kuridhisha sana kwani lengo la BRN limefikiwa kwa asilimia 42 tu.

**Chati ya 1: Hali ya Ufaulu 2012-2013**




**Chanzo: NECTA 2012 - 2013**

**Walimu 3,469(asilimia 18) tu kati ya walimu 19,035 wamepatiwa mafunzo ya Uongozi.**

BRN ya Wizara ya Elimu imebainisha kuwa ukosefu wa mafunzo kwa walimu wakuu huwafanya walimu hao washindwe kusimamia shule na hivyo kuathiri ubora wa elimu itolewayo katika shule zao. Ni dhahiri pia usimamizi bora wa uongozi katika taasisi yoyote ile huleta ufanisi na tija katika kufikia malengo tarajiwa ya taasisi hiyo. Kwa kutambua hilo BRN ilipanga kutoa mafunzo kwa walimu 19,035 kwa shule za msingi na sekondari hadi ifikapo Septemba 2013. Hadi sasa serikali imeweza kuwapatia mafunzo ya uongozi walimu wakuu 3,469 tu. Kwa elimu ya msingi, walimu 2,521 (asilimia 16) tu kati ya 15,525 ndio wamepatiwa mafunzo. Na sekondari walimu 948( asilimia 27) kati ya 3,510 ndio wamepatiwa mafunzo.

**Jedwali la 1: Hali ya Utoaji wa mafunzo kwa walimu**

| | Msingi | Sekondari |
|---|---|---|
| Idadi ya walimu waliotarajiwa kupata mafunzo | 15,525 | 3,510 |
| Idadi ya waliopata mafunzo | 2,521 | 948 |
| Idadi ya ambao hawakupata mafunzo | 13,004 | 2,562 |

Chanzo: URT, (2013) Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa Sekta ya Elimu
Chanzo : Presidential delivery Bureau

**Shule 56(asilimia 7) tu kati ya shule 792 zimejengewa na kukarabatiwa miundombinu**

Kwa mujibu wa lengo la saba la BRN, hadi Septemba 2014 serikali ilipanga kuwa itakuwa imefanya ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwa shule 792. Hadi kufikia Mwezi March 2014 jumla ya shule 56 tu ndizo zilikuwa zimefanyiwa ujenzi na ukarabati wa miundombinu kati ya shule 792. (URT, 2014). Jedwali la 3 linaonesha kuwa jumla ya miundombinu 288 tu ndio imejengwa kwa hizo shule 56 zilizohusishwa. Swali la kujiuliza, linabaki tena, BRN imebainisha kuwa jumla ya miundombinu ya shule 1,200 itajengwa na kukarabatiwa ifikapo Septemba 2015, Je itaweza kufikia lengo hili ikiwa imebaki miezi 12 tu ya utekelezaji. Japo BRN awamu ya kwanza imejikita kwenye ujenzi na ukarabati miundombinu lakini bado kuna changamoto kubwa ya miundombinu kwa shule nyingi. Takwimu za BEST, 2014 zinaonesha kuwa; kwa shule za

sekondari kuna upungufu mkubwa wa maabara za kilimo 1,355(asilimia 94.8), maabara za biolojia 4,416 (asilimia 76.4), maabara za kemia 4,461 (asilimia 72.6) na maabara za fizikia 1.024 (asilimia 75). Pia kuna upungufu wa nyumba za walimu 51,187(asilimia 72), madarasa 13,591(asilimia 22.6) na matundu ya vyoo 44,926(asilimia 40).

Hali ni mbaya zaidi kwa shule za msingi ambapo kuna upungufu wa vyoo 27,736 (asilimia 60.3) ambapo uwiano wa wanafunzi kwa tundu la choo ni 1:53 badala ya 1:25 kwa wavulana na 1:51 kwa wasichana badala ya 1:20. Pia kuna upungufu wa madarasa 82,788( asilimia 41) ambapo uwiano wa wanafunzi kwa darasa ni 1:72 na tatizo ni kubwa zaidi kwa mikoa ya Rukwa(1:84), Geita(1:126) na Mwanza(1:110), upungufu wa nyumba za walimu 161,007(asilimia 79) na madawati milioni 1.2(asilimia 37.7).

**Jedwali la 2: Hali ya Ukarabati wa Shule**

| | Lengo | shule zilizokarabatiwa |
|---|---|---|
| Ifikapo Septemba 2013 | 264 | 56 |
| Ifikapo March 2014 | 528 | 0 |
| Ifikapo Septemba 2015 | 408 | 0 |
| **JUMLA** | **1,200** | **56** |

URT, Jarida la Elimu, Namba 1, 2014

URT, (2013)Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa Sekta ya Elimu

**Jedwali la 3: Hali ya Ujenzi wa Miundombinu hadi July 2014**

| | Aina ya Miundombinu | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Madarasa yaliyojengwa | 44 |
| 2 | Nyumba za walimu zilizojengwa | 10 |
| 3 | Huduma za maji(bomba,kisima) | 14 |
| 4 | Huduma za umeme(kwa shule) | 16 |
| 5 | Matundu ya vyoo yaliyojengwa | 113 |
| 6 | Maabara zilizojengwa | 31 |
| | **JUMLA** | **228** |

Chanzo : Presidential delivery Bureau

kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Shule za msingi zinapaswa kupata sh 10,000[1] kwa kila mwanafunzi na shule za sekondari zinapaswa kupata sh 25,000[2]. Jumla ya Sh billioni 158 zilitarajiwa kukusanywa kwa ajili ya ruzuku ya wanafunzi, lakini katika mwaka wa fedha 2013/2014 ruzuku iliyotolewa ilikuwa ni wastani wa sh 3,580[3] kwa kila mwanafunzi kwa shule za msingi badala ya sh 10,000. Pia kwa shule za sekondari wastani wa sh 16,384 ilitolewa kwa kila mwanafunzi.

Hali hii pia si nzuri na ni ishara hasi kwa BRN kufikia malengo yake ya kuboresha elimu hapa nchini kwa sababu ruzuku ya wanafunzi ndicho chanzo kikuu cha mapato kwa shule nyingi za umma kwa sababu shule nyingi hazina miradi ya kujitegemea na pia hali ya michango ya fedha toka kwa wazazi si nzuri. Ruzuku ya wanafunzi hutumika kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kukidhi gharama ndogondogo za uendeshaji wa shule. Hivyo shule zinapokosa ruzuku, zinashindwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na hivyo kuathiri ubora wa elimu itolewayo shuleni. Jedwali la 3 na 4 yanaonesha picha halisi ya ruzuku iliyotolewa kulingana na lengo.

**Jedwali la 3: Hali ya Ruzuku ya wanafunzi wa Msingi 2013/2014**

| Maelezo | Fedha shs |
|---|---|
| Lengo | 10,000 |
| Ruzuku Iliyotolewa | 3,580 |
| Pungufu | 6,420 |

Chanzo: www.mof.go.tz

**Jedwali la 4: Hali ya Ruzuku ya wanafunzi wa Sekondari 2013/2014**

| Maelezo | Fedha sh |
|---|---|
| Lengo | 25,000 |
| Ruzuku Iliyotolewa | 16,384 |

Chanzo: www.mof.go.tz

[1] Kwa mujibu wa Mpango wa II na wa III wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi
[2] Kwa mujibu wa Mpango wa pili wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari
[3] Takwimu za utoaji wa fedha kwa serikali za mitaa, www.mof.go.tz

Kabla ya utekelezaji wa BRN ya sekta ya walimu, idadi kubwa ya walimu walikuwa watoro wa vipindi ambapo asilimia 53 walikuwa hawahudhurii vipindi wanavyopaswa kufundisha (URT, 2013). Ili kutatua hili, BRN ilidhamiria kuboresha mazingira ya walimu kwa kutoa motisha zisizo za kifedha na kulipa madai ya msingi. Hadi mwezi June mwaka wa fedha 2013/2014 madai ya walimu yalikuwa takribani sh bilioni 62[4]. Hii pia inatoa tafsiri kuwa hata baada ya uwepo wa BRN bado idadi kubwa ya walimu wanaidai serikali na kitendo hiki kitaendelea kuwafanya walimu washindwe kutulia na kuhudhuria vipindi. Utafiti mdogo wa Twaweza wa mwezi June unabainisha kuwa idadi ya walimu kutokuwepo kwenye vipindi umeongezeka toka asilimia 53 mwaka 2013 hadi kufikia asilimia 66 mwaka 2014. Asilimia 34 tu ya walimu ndio wanaingia darasani na kufundisha kwa muda wote wa kipindi.

**Chati ya 2: Mahudhurio ya walimu darasani baada ya BRN**




Chanzo: Twaweza, Sauti za Wananchi, brief 13, 2014

[4] HakiElimu brief 2014 na HakiElimu press statement 2014, Speech, Shadow Minister for Education, 2014

Chati ya 3: Mahudhurio ya walimu kabla ya BRN




URT, (2013) Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa Sekta ya Elimu

**Hitimisho na Mapendekezo**

Hali ya utekelezaji wa BRN si ya kuridhisha. Kijarida hiki kimeonesha hali halisi ya utekelezaji kwa kila lengo.Utekelezaji wa kusuasua wa BRN bado umeendelea kuathiri mazingira ya kufundishia na kujifunzia na hivyo kuathiri ubora wa elimu itolewayo kwa wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari. Ufaulu bado uko chini ya asilimia 60 kwa elimu ya sekondari na chini ya asilimia 50 kwa elimu ya msingi, bado idadi kubwa ya walimu hawajapatiwa mafunzo ya uongozi na ufundishaji wa KKK, hali ya utoaji wa fedha za ruzuku si mzuri ambapo kwa wastani shule za msingi zinapata sh 3,580 kwa wastani badala ya sh 10,000 kwa kila mwanafunzi na sekondari zinapewa sh 16,384 kwa wastani badala ya sh 25,000 kwa kila mwanafunzi na hali ya miundo mbinu kwa shule nyingi si ya kuridhisha.

Serikali isijidanganye na ufaulu huu unaonekana kupanda ghafla kwani changamoto zilizopo katika elimu ni nyingi na bado hazijatatuliwa. Mfano mzuri ni migogoro ya mara kwa mara kati ya walimu na mwajiri wao kuhusu malipo mbalimbali hali iliyosababisha walimu kuwa watoro, ukosefu wa maabara, vifaa vya kufundishia na tofauti kubwa iliyopo katika gharama za utoaji elimu

nchini kati ya shule za serikali na shule za binafsi. Kwa ujumla bado shule nyingi hazina miundombinu rafiki, walimu na vitendea kazi vya kutosha kupata matokeo mazuri katika kipindi kifupi kilichopangwa katika BRN. Mpango wa BRN ni mzuri lakini muda uliowekwa kutekeleza malengo yake ni mfupi kwa kuzingatia mazingira ya utoaji elimu na changamoto zake. Pia kumekuwepo na mabadiliko ya mara kwa mara katika sekta ya elimu likiwemo la hivi karibuni la alama za ufaulu. Mabadiliko ya viwango vya upimaji wa matokeo ya wanafunzi vinaweza kuongeza ufaulu tu na si ubora wa elimu.

Matokeo mazuri yoyote ya mipango ya maendeleo ikiwemo elimu yanahitaji uwekezaji wa kutosha. Shule za msingi na sekondari zina changamoto nyingi za upungufu wa miundombinu. Serikali haina budi kutafakari na kuona kama uwekezaji uliofanyika mpaka sasa umefanyika kiasi cha kutosha kuleta matokeo kusudiwa. Hali ya uwekezaji kwenye sekta ya elimu si nzuri ambapo asilimia 24 tu ya fedha ya bajeti inapangwa kwenye miradi ya maendeleo inayohusu miundominu ilihali matumizi ya kawaida yakiwa asilimia 74 ya bajeti ya elimu.

Ili kutekeleza Matokeo Makubwa Sasa hatuna budi kujifunza toka kwa nchi zilizofanikiwa kutekeleza mipango kama Malaysia kwamba; Matokeo Makubwa Sasa maana yake ni viongozi kufanya tofauti na wafanyavyo sasa, kuwajibika kwa hali ya juu, viongozi kuwa wabunifu, viongozi kupanga mipango na kuitafutia fedha za utekelezaji, viongozi kufanya kazi na kutenda ili kutekeleza wayanenayo kwa ajili ya kupata matokeo ya haraka.

HakiElimu inawezesha
wananchi kuleta mabadiliko
katika elimu na demokrasia

SL P 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu. (255 22) 2151852/3 • Faksi (255 22) 215244
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org

hakielimu